**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA, MHESHIMIWA BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UZINDUZI WA MPANGO WA PAMOJA WA USHIRIKIANO KATI YA WAAJIRI NA VYUO

**JNICC, DAR ES SALAAM**
**9 FEBRUARI, 2026**

- ***Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;***
- ***Mhe. Lela Mohamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar;***
- ***Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam;***
- ***Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta kutoka wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;***
- ***Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;***
- ***Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama;***
- ***Mhe. Balozi Dkt. Asha Rose Migiro, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Taifa na viongozi wote wa Chama;***
- ***Mhe. Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali;***
- ***Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia & Makatibu Wakuu kutoka Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;***
- ***Mhe. Husna Juma Sekiboko (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo & Wahe. Wabunge wote mliohudhuria;***
- ***Wawakilishi wa Benki ya Dunia na Wadau wa Maendeleo;***
- ***Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;***
- ***Wawakilishi wa Sekta Binafsi na Waajiri;***
- ***Watendaji Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi;***
- ***Wawakilishi wa Wanafunzi;***
- ***Waandishi wa habari;***
- ***Wageni waalikwa,***
- ***Mabibi na Mabwana;***

**Kazi na Utu…!**

Tumekutana leo katika tukio hili muhimu kwa mustakabali wa elimu, rasilimaliwatu na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla. Tukio hili linatokana na dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha elimu inayotolewa inachochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. Hivyo, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyewezesha jambo hili na kutuwezesha sisi kukusanyika hapa tukiwa wenye afya njema.

Uzinduzi wa Mpango huu ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, ambapo aliahidi kuanzisha Mpango wa pamoja kati ya Waajiri, Vyuo vya ufundi stadi na Vyuo Vikuu kwa lengo la kulinganisha mafunzo na mahitaji halisi ya sekta za kipaumbele za Taifa, ndani ya siku 100 baada ya

kuapishwa kwake. Hivyo, naipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wake kwa kutekeleza ahadi hii.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Kama ilivyokwishaelezwa, Mpango huu unashirikisha Waajiri, Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, na unalenga kuleta mageuzi makubwa katika mfumo wetu wa elimu na mafunzo. Pamoja na mambo mengine, Mpango unalenga kuimarisha uhusiano wa kimkakati kati ya utoaji wa elimu na utendaji kazi, kwa lengo la kulinganisha mafunzo na mahitaji ya sekta za kipaumbele kama nishati, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na viwanda vya kuongeza thamani. Aidha, Mpango unaweka msingi thabiti wa kujenga kizazi cha wahitimu wenye uwezo wa kuajirika, kujiajiri na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa kwani umedhamiria kubadilisha mfumo wa elimu ya nadharia kwenda mfumo unaozingatia ujuzi, vitendo, ubunifu na uzalishaji mali. Kimsingi, Mpango huu unasisitiza mageuzi kuelekea mafunzo yanayozingatia umahiri, ushirikishwaji mpana wa sekta ya uzalishaji, na uwiano wa karibu kati ya utoaji wa elimu na vipaumbele vya kiuchumi vya Taifa. Mpango utatekelezwa sambamba na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2023, pamoja na ajenda ya mageuzi ya elimu ya Zanzibar.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Serikali ya Awamu ya Sita imeweka kipaumbele cha kimkakati katika kukuza ujuzi, stadi, maarifa na sifa za kuajirika au kujiajiri miongoni mwa vijana na wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, ikitambua kwamba maendeleo endelevu ya Taifa hayawezekani bila kuwa na rasilimaliwatu iliyoelimika na yenye uwezo wa kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa. Dhamira hii inatokana na ukweli kwamba 34.5% ya Watanzania ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 35, wanaohitaji kuandaliwa kwa ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira la kitaifa na kimataifa, ambapo kwa sasa zaidi ya wanafunzi milioni 2.1 wapo katika taasisi za elimu ya juu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, jambo linaloipa Serikali na wadau wake wajibu wa kuhakikisha mfumo wa elimu unazalisha wahitimu wenye umahiri, wanaoweza kuajiriwa au kujiajiri na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya Taifa.

Katika muktadha huo, Serikali imeendelea kufanya maboresho makubwa ya sera na mitaala ya elimu katika ngazi zote kwa lengo la kuujenga mfumo wa elimu ulio mnyumbufu, jumuishi na unaoendana na vipaji, mwelekeo na mahitaji halisi ya soko la ajira, huku ikizingatia mabadiliko ya teknolojia na ushindani wa kitaifa na kimataifa. Vilevile, Serikali imeendelea kutenga rasilimali kubwa katika sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi kwa kuongeza bajeti ya elimu mwaka hadi mwaka, fedha ambazo zimeelekezwa katika ujenzi na uboreshaji wa vyuo, karakana na maabara, pamoja na kuwezesha

mafunzo ya vitendo yanayohusisha sekta binafsi. Uwekezaji huu wa kimkakati unalenga kuifanya elimu kuwa injini muhimu ya ukuaji wa uchumi, ubunifu na ajira endelevu nchini.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Kisera, Mpango huu wa kimkakati unashabihiana na malengo ya mipango ya maendeleo ya Serikali. Utekelezaji wake ni ukamilishaji wa ahadi iliyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025–2030 ya kutengeneza ajira 8,084,203 kwa upande wa Tanzania Bara na ajira za vijana 350,000 kwa upande wa Zanzibar, ifikapo 2030; Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inayolenga kupandisha wastani wa kipato cha mtanzania kufikia uchumi wa kipato cha dola za Marekani 7,000, pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 inayolenga kupunguza ukosefu wa ajira kutoka 14.1% hadi 6.2%. Dira zote kwa pamoja zinasisitiza umuhimu wa ukuzaji wa ujuzi, ajira kwa vijana, na uhusiano thabiti kati ya elimu na soko la ajira.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Nimefurahi kusikia kuwa maandalizi ya Mpango huu yamejumuisha mashauriano ya kina yaliyohusisha wanataaluma, sekta binafsi, waajiri, viwanda, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa huduma za elimu, na wadau wa maendeleo. Wizara pia imeshirikiana na wadau hao katika uandaaji wa pamoja wa mitaala, utoaji wa mafunzo kwa vitendo, utafiti wa pamoja, ushauri wa kitaalam na uanagenzi. Lengo likiwa ni kuimarisha mfumo wa elimu kwa kufungamanisha mafunzo na mahitaji ya ujuzi katika soko la ajira kwa kubainisha muundo thabiti unaoweka uwajibikaji wa pamoja, na ushirikishwaji wa waajiri. Kupitia Mpango huu ushirikiano utaimarishwa, kusimamiwa na kupimwa ili uwe na matokeo yanayopimika katika ubora wa mafunzo, ajira za wahitimu na mchango wa elimu katika ukuaji wa Uchumi wa Taifa.

Kwingineko duniani, uzoefu unaonesha kuwa mifumo rasmi ya ushiriki wa waajiri, ufadhili unaotabirika, na mafunzo yanayozingatia ujuzi huongeza kwa kiasi kikubwa matokeo ya ajira. Aidha, majukwaa ya kitaifa yanayounganisha elimu, ajira na ujuzi endelevu ni muhimu katika kuimarisha ushindani wa uchumi.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Ushirikiano baina ya taasisi za elimu na viwanda ni hitaji la lazima katika dunia ya leo. Vyuo haviwezi tena kuwa visiwa vya nadharia, na viwanda haviwezi kukua bila nguvukazi yenye ujuzi unaoendana na teknolojia na ushindani wa soko. Sekta ya viwanda inategemewa sana katika kufanikisha mapitio ya mitaala, utoaji wa mafunzo kwa vitendo, uanagenzi na kusaidia kubaini ujuzi unaohitajika sasa na baadaye. Hivyo, nitumie fursa hii kushukuru na kupongeza wadau na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoshirikiana na Serikali katika malezi na maendeleo ya vijana. Kipekee, natambua mchango mkubwa wa taasisi za dini nchini, ambazo zimeendelea kutoa malezi bora, elimu ya maadili na ujuzi

wa kujitegemea kwa vijana kupitia makongamano, semina na taasisi zao za elimu. Mchango huu ni muhimu katika kujenga kizazi chenye maadili, ujuzi na uzalendo.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Washiriki;***
Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kusisitiza masuala matatu ambayo kwa mtazamo wangu yatasaidia kufanikisha utekelezaji wa mpango huu, kama ifuatavyo:

**Kwanza,** ni kuhusu umuhimu wa tafiti na ubora wa elimu kwa ujumla. Ili kuinua viwango vya tafiti na na ubora wa elimu, napenda kutoa wito kwa sekta binafsi kushirikiana na vyuo kuwekeza katika tafiti hususan za sayansi na teknolojia na kuhimiza ubunifu katika ufundishaji na ujifunzaji. Kupitia Mpango huu, Sekta binafsi inaweza kuchangia maendeleo ya elimu yetu kwa kufadhili tafiti na kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa fani mbalimbali kulingana na mahitaji ya soko la ajira.

**Pili,** ni Mafunzo kwa vitendo. Ushiriki wa Waajiri na Wenye viwanda katika utekelezaji wa Mpango huu ni muhimu hususan katika uandaaji na mapitio ya mitaala; fursa za mafunzo kwa vitendo, uanagenzi na mafunzo kazini; ushiriki wa wataalamu viwandani katika ufundishaji; tathmini ya wanafunzi na uthibitishaji wa ujuzi; na uimarishaji wa miundombinu ya mafunzo. Ushirikiano huo utawezesha sekta binafsi kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo *(field practical training)*; na mafunzo kazini (*internships)* kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na waajiriwa wa fani mbalimbali.

**Tatu,** ni wito kwa taasisi za elimu na sekta binafsi nchini kuzingatia maendeleo ya kasi ya sayansi na teknolojia duniani katika utekelezaji wa Mpango huu. Vyuo na sekta binafsi vishirikiane kubaini ujuzi muhimu unaohitajika sasa na siku zijazo hususan katika fani za: sayansi; teknolojia; ubunifu; tiba; uhandisi; na hesabu ili kuwezesha vijana wetu kushindana na kupata nafasi katika soko la ajira hapa nchini na kimataifa.

Mwisho, ninatoa rai kwa wadau wote kuhakikisha kuwa Mpango huu unaozinduliwa leo unatekelezwa kwa vitendo. Ni matarajio ya Serikali kuona matokeo yanayopimika katika ubora wa mafunzo, ajira za vijana, ubunifu wa teknolojia na ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Baada ya kusema hayo, ninayo heshima sasa kutamka kuwa Mpango wa pamoja wa Ushirikiano kati ya Waajiri na Vyuo, umezinduliwa rasmi.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**